SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY (MBM) KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Mei, 2015

YALIYOMO

A. UTANGULIZI.....1

B. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2014/2015.....2

B1 IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI.....3

B2 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI.....6

B3 MAHKAMA.....8

B4 AFISI YA MWANASHERIA MKUU.....12

B5 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA.....13

B6 AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA.....16

B7 AFISI YA MUFTI.....18

B8 WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI.....21

B9 AFISI YA MRAJIS WA VIZAZI NA VIFO.....23

B10 AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI.....25

B11 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA.....27

B12 AFISI KUU PEMBA.....30

C. MWELEKEO WA MATUMIZI YA BAJETI INAYOTUMIA PROGRAMU.....32

Fungu G01 - Wizara ya Katiba na Sheria.....32

Fungu G02 - Mahkama.....33

Fungu G03 – Mwanasheria Mkuu wa Serikali.....34

Fungu G04 – Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.....34

Fungu G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria.....35

D. SHUKURANI.....35

E. HITIMISHO.....37

VIAMBATISHO

Kiambatanisho1:Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2014/15.....38

Kiambatanisho 2: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2015/16...43

Kiambatanisho3: Makusanyo ya Mapato na Makadirio ya 2015/2016 45

Kiambatanisho 4: Miradi ya Maendeleo 2015/16.....46

Kiambatisho 5a:- Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2014/2015.....47

Kiambatanisho 5b: Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Mwanzo na Kadhi 2014/15.....49

Kiambatanisho 6: Miswada – Afisi ya Mwanasheria Mkuu 2014/15.....50

Kiambatanisho 7a: Mapato – Wakala wa Usajili Biashara na Mali 2014/15.....51

Kiambatanisho 7b: Mapato – Ofisi ya Mrajis Vizazi na Vifo 2014/15.....52

Kiambatisho 8: Vikundi vilivyosafirisha Mahujaji 2014 - KWNMA.....53

Kiambatisho 9: Usajili wa Kazi za Hakimiliki.....54

Kiambatanisho: 10a Idadi ya Wafanyakazi wa Wizara 2014/2015.....55

Kiambatanisho 10b: Idadi ya Wafanyakazi Waliopo Mafunzoni 2014/15.....56

HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA MHESHIMIWA ABUBAKAR KHAMIS BAKARY (MBM) KWENYE BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

A. UTANGULIZI

1. **Mhe. Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kujadili na hatimaye kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

2. **Mhe. Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutuwezesha kukutana tena katika hali ya uzima kwenye mkusanyiko huu muhimu katika kutekeleza jukumu letu la kitaifa la kujadili maendeleo ya nchi yetu.

3. **Mhe. Spika,** baada ya shukurani hizo naomba nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein, kwa uongozi wake wa busara unaomwezesha kuiongoza nchi yetu katika hali ya amani.

4. **Mhe. Spika,** naomba pia nichukue fursa hii kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, na Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa kazi kubwa wanazofanya katika utekelezaji wa majukumu yao, ikiwemo kumshauri Mheshimiwa Rais, ambayo wanaitekeleza kwa ufanisi mkubwa.

5. **Mhe. Spika,** naomba uniruhusu kutoa pongezi kwako kwa kuliongoza vyema Baraza letu na kwa ufanisi mkubwa. Vilevile, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza watendaji wa Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu wa Baraza kwa kuifanya kazi yako ya kuliongoza Baraza hili kuwa ya mafanikio.

6. **Mhe. Spika,** naomba pia nitoe shukurani maalum na za pekee kwa Wajumbe wa Kamati za Baraza kwa jumla kwa kutekeleza majukumu yao kwa umahiri mkubwa. Aidha, natoa shukurani kwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kuishauri ipasavyo Wizara ya Katiba na Sheria katika mambo mbalimbali, chini ya uongozi imara wa Mwenyekiti Mheshimiwa Ussi Jecha Simai. Napenda pia kuishukuru Kamati ya PAC kwa ushirikiano wanaotoa kwa wizara, ambao ni nyenzo muhimu inayosaidia uwajibikaji katika masuala ya fedha.

7. **Mhe. Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naomba uniruhusu niwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Mgogoni kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa pamoja na imani yao kwangu ambavyo vimeniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Serikali pamoja na ya jimbo kwa mafanikio.

B. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2014/2015

8. **Mhe. Spika,** katika mwaka 2014/15, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa jumla ya shilingi 10,244,164,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 6,551,455,000.00 zilipangwa kulipia mishahara na stahiki mbalimbali za watumishi na shilingi 3,692,709,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2015 jumla ya shilingi

6,589,077,001.00 (61%) zimepatikana. Kati ya fedha hizo, shilingi 4,861,750,000.00 (74%), kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi, na shilingi 1,727,327,001.00 (47%) kwa matumizi mengineyo. Vilevile, wizara ilikadiriwa kutumia ruzuku ya shilingi 765,300,000.00 na hadi kufikia Machi 2015 imepokea shilingi 542,540,611.00 (71%). Aidha, kwa kazi za maendeleo shilingi 2,679,748,700.00 ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,100,000,000.00 ni Mchango wa Serikali na shilingi 1,579,748,700.00 ni msaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2014, shilingi 945,530,050.00 (35%) zimepatikana, ambapo shilingi 315,000,000.00 (29%) ni Mchango wa Serikali na shilingi 630,530,050.00 (40%) zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo. Wizara pia ilikadiria kukusanya shilingi 442,494,000.00 ili kuchangia mapato ya Serikali. Hadi Machi 2015, fedha zilizokusanywa ni shilingi 389,396,692.00 (88%) (Viambatanisho nam. 1&3 vinahusika).

9. **Mhe. Spika,** sasa naomba nitoe taarifa ya shughuli za Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2014/15 kwa kueleza maendeleo ya utekelezaji wa malengo ya wizara kama ifuatavyo:-

B1 IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

10. **Mhe. Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina jukumu la kusimamia na kuratibu masuala ya mipango, miradi, sera na utafiti. Katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Idara imetekeleza jukumu lake kwa kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi za wizara za kila robo mwaka na taarifa za usimamizi wa miradi ya maendeleo na kuziwasilisha kwenye mamlaka na vikao vinavyohusika. Pia, katika kuratibu na kutekeleza

mipango ya wizara na taasisi zake, Idara imefanya uratibu wa matayarisho ya mipango ya kibajeti ikiwemo mpango wa matumizi wa muda wa kati (MTEF) na bajeti inayotumia programu (Programme Based Badget - PBB). Aidha, Idara imeendelea kuratibu utekelezaji wa mpangokazi wa wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na kukusanya na kuweka pamoja taarifa za utekelezaji bajeti ya wizara, pamoja na taarifa za miradi ya maendeleo.

11. **Mhe. Spika,** Idara pia imeratibu Programu ya Mabadiliko Katika Sekta ya Sheria; Mradi wa Kuimarisha Ofisi ya Mkurugenzi Mashtaka; Mradi wa Kuimarisha Usajili na Upatikanaji wa Takwimu za Matukio ya Kijamii; na Mradi wa Kuimarisha Majengo ya Mahkama. Utekelezaji wa miradi hiyo uko katika hatua mbalimbali na ufafanuzi wa taarifa zake utatolewa kwenye taasisi zinazohusika.

12. **Mhe. Spika,** pamoja na kazi hizo, Idara imefanya maandalizi ya kazi za utafiti na sera kwa kuratibu utafiti wa taarifa za msingi za sekta ya sheria (Legal Sector Baseline Study) na utafiti kuhusu njia bora ya utunzaji wa kumbukumbu. Idara pia imeandaa sera ya msaada wa kisheria. Rasimu ya sera hiyo inaendelea kufanyiwa mapitio wizarani na kuwekwa tayari kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye vikao vinavyohusika. Aidha, kupitia mradi wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria, Idara imeratibu utoaji wa mafunzo kuhusu uhalifu wa kimtandao, mikataba, utafiti na uandishi wa ripoti za sheria; na utafiti juu ya usimamizi wa kesi. Aidha, yamefanyika mapitio ya mwongozo wa uendeshaji mashtaka; kuhuisha tovuti ya wizara; na ununuzi wa vitabu na ripoti za sheria.

13. **Mhe. Spika,** Idara vilevile imeratibu mapitio ya Sheria ya Ushahidi na Sheria ya Madai; imeandaa mpangokazi wa mwaka mmoja wa utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko Katika Sekta ya Sheria; imeratibu maandalizi ya utafiti wa msingi kwa ajili ya uwezekano wa kununua mashine ya uchunguzi wa vinasaba (Deoxyribo Nucleic Acid - DNA), na inaendelea kuratibu matayarisho ya nyaraka za miradi ya maendeleo itakayokwenda sambamba na Programu ya Mabadiliko katika Sekta ya Sheria. Aidha, Idara imesimamia mradi wa ujenzi wa jengo la wizara huko Mazizini ambao umekamilika. Hata hivyo, mradi huo haukukamilika kwa wakati uliopangwa kutokana na upungufu wa fedha za malipo ya Mkandarasi.

14. **Mhe. Spika,** Idara iliendelea kuwapatia stahiki wafanyakazi wake watano walioko masomoni katika ngazi ya shahada ya uzamili, na shahada ya kwanza. Kati ya hao mfanyakazi mmoja ameripoti kazini baada ya kumaliza masomo yake katika ngazi ya stashahada ya uzamili.

15. **Mhe. Spika,** katika mwaka 2014/15 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa shilingi 224,252,000.00 ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 128,784,000.00 kwa ajili ya mishahara na stahiki kwa watumishi na shilingi 95,468,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2015, shilingi 109,567,550.00 (49%) zimepatikana. Kati ya fedha hizo, shilingi 84,923,500.00 (66%) zimetumika kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 24,644,050.00 (26%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 1,729,748,700.00 ziliidhinishwa kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2015, fedha zilizopatikana ni shilingi 680,530,050.00 (39%). Kati ya fedha hizo, shilingi

50,000,000.00 (33%) ni kutoka Serikalini na shilingi 630,530,050.00 (40%) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (Viambatanisho Nam 1&2 vinahusika).

B2 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

16. **Mhe. Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina dhamana ya kusimamia na kuratibu shughuli zote za uendeshaji na utumishi kwa idara na taasisi za wizara. Katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeendelea kuzifanyia mapitio taarifa za watumishi, kuzirekebisha na kuziingiza katika "data base" ya wizara. Vilevile, Idara imesimamia shughuli za uajiri na kutayarisha mafao ya wastaafu. Jumla ya wafanyakazi wanane wameajiriwa katika taasisi za wizara na tayari wameanza kazi. Idara pia imeratibu mipango ya mafunzo na kumbukumbu za ofisi na za wafanyakazi. Aidha, Idara kwa kushirikiana na Wizara Nchi (AR) Kazi na Utumishi wa Umma imefanikisha kazi ya kurekebisha mishahara ya wafanyakazi wenye uzoefu.

17. **Mhe. Spika,** Idara imeandaa mikutano miwili ya Kamati ya Uongozi, mikutano mitano ya Kamati Tendaji, na vikao sita vya Bodi ya Zabuni. Vilevile, Idara imeendelea kusimamia kazi ya kuandaa Mkataba wa Utoaji wa Huduma kwa Mteja kwa kufanya vikao vya kazi vitano vya Kamati ya Utumishi ya Wizara. Pamoja na shughuli hizo, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inasimamia utendaji wa vitengo vinne vya Wizara ambavyo ni:- Ukaguzi wa Ndani, Uhasibu, Ununuzi na Kitengo cha Mwasiliano.

18. **Mhe. Spika,** kazi za ukaguzi wa ndani wa hesabu zimefanyika kwa ufanisi ambapo Ripoti za Ukaguzi za Julai – Septemba na Oktoba – Disemba 2014/15 zimewasilishwa kwenye Kamati ya Ukaguzi ya Wizara na kujadiliwa. Ripoti ya Januari – Machi 2015 ipo kwenye hatua ya maandalizi. Kwa upande mwingine, Kitengo cha Uhasibu kimetekeleza kazi zake za kawaida ikiwemo kutoa ufafanuzi wa hoja za Wakaguzi wa Hesabu, kuandaa ripoti ya mwaka ya upatikanaji wa fedha (Financial Statement) na kuiwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

19. **Mhe. Spika,** Idara imeendelea na usimamizi wa upatikanaji wa vitendea kazi pamoja na huduma muhimu za uendeshaji wa ofisi ikiwemo huduma za mawasiliano, usafiri, vitendea kazi, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la ofisi. Idara pia imeratibu masuala ya upatikanaji wa habari kwa kutoa mafunzo kwa Kamati ya Uhariri ya taarifa za mtandao, kutayarisha matangazo ya TV, vipeperushi vya Mkakati wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria na mikutano ya Mhe. Waziri na Waandishi wa Habari.

20. **Mhe. Spika,** katika kuratibu masuala mtambuka, Idara imeendesha mafunzo maalum kwa Maafisa wa Wizara juu ya masuala yanayohusu shughuli za Watu Wenye Ulemavu na mapambano dhidi ya UKIMWI na mazingatio yake katika mipango ya kazi.

21. **Mhe. Spika,** Idara imeendelea kuwalipia gharama za masomo wafanyakazi wawili wanaoendelea na masomo katika ngazi ya shahada ya uzamili ya sheria na shahada ya rasilimali watu. Aidha, wafanyakazi wawili wamehudhuria

mafunzo ya muda mfupi nchini India na Tanzania Bara kwa ajili ya kuongeza ufanisi.

22. **Mhe. Spika,** katika Mwaka 2014/15, Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 716,161,000.00 kwa kazi za kawaida ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 465,723,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 250,438,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2015 fedha zilizopatikana ni shilingi 392,275,000.00 (55%). Kati ya fedha hizo, shilingi 287,680,750.00 (62%) zilitumika kulipia mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 104,594,250.00 (42%) kwa matumizi mengineyo (Kiambatanisho Nam. 1 kinahusika).

B3 MAHKAMA

23. **Mhe. Spika,** Mahkama ina jukumu la kusimamia utoaji wa haki. Katika kufanikisha jukumu hilo Mahkama imesikiliza kesi mbalimbali za madai na jinai pamoja na rufaa za Mahkama Kuu. Kwa kipindi cha Julai - Machi 2014/15 Mahkama imepokea na kusajili kesi 6783 kutoka Mahkama zote Unguja na Pemba.

24. **Mhe. Spika,** katika kipindi hicho, Mahkama Kuu imepokea mashauri mapya 163. Ukijumuisha na mashauri 116, imekuwa na jumla ya mashauri 279. Mashauri manne yametolewa uamuzi. Katika Divisheni ya Mahkama ya Kazi, yamepokelewa mashauri mapya 11 na kuifanya divisheni hiyo iwe na mashauri 18 kwa kujumuisha na mashauri saba yaliyosajiliwa kabla. Hakuna mashauri yaliotolewa maamuzi katika mahkama hiyo.

25. Mhe. Spika, katika Mahkama za Mkoa, mashauri mapya 221 yamepokelewa na kufanya Mahkama hizo ziwe na jumla ya mashauri 537, kwa kujumuisha na mashauri mengine 316 yaliyosajiliwa kabla. Mahkama za Mikoa zimetoa maamuzi kwa mashauri 47.

26. Mhe. Spika, kwa upande mwengine, Mahkama za Wilaya zilipokea mashauri mapya 2,504 na kufikisha jumla ya mashauri 4,893 yanapojumuishwa na mashauri 2,389 yaliyosajiliwa kabla. Katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015, Mahkama hizo zimetolea uamuzi mashauri 1,865.

27. Mhe. Spika, Mahkama za Mwanzo zilipokea mashauri mapya 2,783 na kufikisha jumla ya mashauri 5,385 yanayojumuisha mashauri 2,602 yaliyosajiliwa kabla. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2015 Mahkama hizo zimetolea uamuzi mashauri 2,448.

28. Mhe. Spika, Mahkama ya Kadhi wa Rufaa imepokea mashauri mapya 37, na kuifanya iwe na jumla ya mashauri 72 yanapojumuishwa na mashauri 38 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 17 kati ya hayo yametolewa uamuzi. Vilevile, Mahkama za Kadhi wa Wilaya zilipokea mashauri mapya 1,033 na kuwa na jumla ya mashauri 2,013 yanapojumuishwa na mashauri 980 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 459 kati ya hayo yametolewa uamuzi.

29. Mhe. Spika, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania kwa mwaka wa fedha 2014/15 ilikuwa na idadi ya mashauri kumi yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma. Kufikia Machi 20145 Mahkama hiyo imepokea mashauri sita na kufikisha jumla

ya mashauri 16. Hadi kufikia Machi 2015 jumla ya mashauri sita yalitolewa uamuzi.

30. **Mhe. Spika,** Mahkama ya Watoto ilianza mwaka wa fedha 2014/15 ikiwa na idadi ya mashauri 23 yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma na kupokea mashauri mapya 28 na hivyo kufanya idadi ya mashauri kufikia 51. Katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015 Mahkama ya Watoto imetoa uamuzi kwa mashauri 9. Uchache huo unatokana na kukosekana kwa mashahidi.

31. **Mhe. Spika,** kwa uchambuzi huo, Mahkama imepokea na kusajili jumla ya mashauri 6,783 kutoka mahkama zote kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015 ambapo idadi ya mashauri yaliyosikilizwa na kutolewa uamuzi ni 4,854 sawa na 72% (Viambatanisho nam. 5a & 5b vinahusika).

32. **Mhe. Spika,** ili kupunguza mrundikano wa kesi, Mahkama imeendelea na utaratibu wake wa kukutana na wadau wa kesi kupitia kamati yake ya kusukuma kesi ambapo vikao viwili vilifanyika. Vilevile UNICEF kupitia Mpango wa Mabadiliko Katika Haki za Mtoto iliwapatia mafunzo baadhi ya Majaji, Mahakimu na Makarani wa Mahkama juu ya namna ya kutumia kanuni za Mahkama za watoto na jinsi ya kushughulikia kesi za watoto.

33. **Mhe. Spika,** katika kuelimisha jamii, Mahkama imechapisha na kusambaza kwa wananchi toleo la 3 la Jarida la Mahkama na kuendesha vipindi kupitia televisheni ya ZBC. Katika kusherehekea maadhimisho ya nne ya Siku ya Sheria Zanzibar (Law Day), Mahkama ilifanya mdahalo uliowekea msisitizo kaulimbiu ya "Mahkama huru ni msingi wa utawala bora."

34. **Mhe. Spika,** katika kuwajengea uwezo wafanyakazi wake, Mahkama imewapatia fursa ya masomo wafanyakazi tisa katika fani za utawala, uwekaji wa kumbukumbu na sheria. Aidha, ili kuwezesha shughuli za kila siku za Mahkama, mahitaji na vitendea kazi vya ofisi vimenunuliwa.

35. **Mhe. Spika,** Mahkama imeendelea kuimarisha majengo yake kwa kuanza matengenezo ya jengo la Mahkama Chake Chake Pemba. Matengenezo yaliyokwishafanyika ni pamoja na kuezekwa kwa jengo lote na kurekebisha mfumo wa umeme. Matarajio ni kuendelea na ujenzi huo hali ya upatikanaji wa fedha itakaporuhusu.

36. **Mhe. Spika,** katika mwaka wa fedha 2014/15, Mahkama iliidhinishiwa jumla ya shilingi 5,036,700,000.00 kwa kazi za kawaida zikiwemo shilingi 3,536,700,000.00 kwa mishahara na stahiki, na shilingi 1,500,000,000.00 kwa matumizi mengineyo. Jumla ya shilingi 700,000,000.00 ziliidhinishwa kwa kazi za Maendeleo na kupitia Mpango wa Mabadiliko Katika Haki za Mtoto, Mahkama ilipatiwa jumla ya shilingi 55,242,000. Aidha, shilingi 95,000,000.00 zilikadiriwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya Serikali.

37. **Mhe. Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2015 Mahkama iliingiziwa shilingi 3,325,366,205.00 (66%) kwa matumizi ya kazi za kawaida, zikiwemo shilingi 2,739,663,400.00 (77%) zilizotumika kulipia mishahara na stahiki za wafanyakazi na shilingi 585,702,805.00 (39%) kwa matumizi mengineyo. Kwa kazi za maendeleo, Mahkama iliingiziwa shilingi 200,000,000.00 (29%) kutoka Serikalini. Shilingi 128,346,107.00 (135%) zimekusanywa kuchangia mapato ya Serikali (Kiambatanisho nam. 1 & 3 kinahusika.)

B4 AFISI YA MWANASHERIA MKUU

38. **Mhe. Spika,** jukumu la msingi la Afisi ya Mwanasheria Mkuu ni kuishauri Serikali kwa mambo ya kisheria ikiwemo kuandaa mikataba ya kitaifa na kimataifa, kutayarisha miswada ya sheria, kusimamia mashauri ya madai kwa niaba ya serikali na kuandaa hati na nyaraka za kisheria.

39. **Mhe. Spika,** katika mwaka wa fedha 2014/15, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imetayarisha rasimu za miswada ya sheria nne kwa lengo la kupata sheria mpya ambazo baadhi yao zimepitwa na wakati na nyengine zilikuwa hazipo kabisa. Lengo ni kuweka nguvu za kisheria katika masuala ya uwakala na usimamizi wa amana na wasia (Kiambatanisho Nam. 6.) Vilevile, Afisi imeandaa na kuchapisha kanuni za sheria mbalimbali, matangazo ya kisheria (Legal Notice), imesimamia mikataba 50 kwa ajili ya wizara na taasisi za Serikali na hati za maelewano (MOU) yaliyoingiwa na Serikali. Wakati huo huo, Afisi inaendelea kusimamia kesi 60 za madai zilizofunguliwa dhidi ya Serikali.

40. **Mhe. Spika,** Afisi ya Mwanasheria Mkuu imekusanya na kuyaweka pamoja magazeti rasmi ya serikali kuanzia mwaka 1910 hadi mwaka 1955. Kazi hiyo inaendela na lengo ni kukusanya magazeti rasmi hadi kufikia mwaka 1963.

41. **Mhe. Spika,** ili kutekeleza masharti ya kifungu cha 11 cha Sheria namba 6 ya 2013 ya Kuanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Afisi imeanza kuwateuwa Maafisa Sheria kumi na tano kutoka wizara za SMZ kuwa Mawakili wa Serikali ili kushirikiana na wanasheria kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika kutekeleza majukumu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

42. Mhe. Spika, Afisi siliandaa warsha kuhusiana na utakasishaji wa fedha haramu kwa lengo la kutoa uwelewa kwa watendaji wake pamoja na mahakimu, maafisa sheria wa taasisi mbalimbali za Serikali na watendaji kutoka taasisi za fedha nchini. Kwa upande mwingine, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeendelea kuwasomesha watendaji wake ambapo wafanyakazi wanne wamepatiwa mafunzo katika fani ya sheria na utawala kwa kiwango cha shahada na stashahada. Kupitia Programu ya Mabadiliko Katika Sekta ya Sheria, Afisi pia imewapatia mafunzo wanasheria wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Maafisa Sheria kutoka wizara na taasisi mbalimbali za serikali, yanayohusiana na masuala ya mikataba na utatuzi wa migogoro.

43. Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/15 Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliidhinishiwa shilingi 999,300,000.00 zikiwemo shilingi 461,900,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 537,400,000.00 kwa matumizi mengineyo. Kufikia Machi 2015, jumla ya shilingi 621,349,575.51 (62%) zilipatikana zikiwemo shilingi 311,192,025.00 (67%) kwa ajili ya mishahara na shilingi 310,157,550.51 (58%) kwa matumizi mengineyo (Kiambatanisho nam. 1 kinahusika).

B5 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

44. Mhe. Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ina jukumu la kuzifanyia mapitio Sheria za Zanzibar na kupendekeza marekebisho yake. Utekelezaji wa jukumu hilo unahusisha utafiti na kuwashirikisha wananchi katika hatua mbalimbali hadi kupendekeza marekebisho ya sheria zinazohusika. Tume pia inatoa elimu kwa umma juu ya

Sheria za Zanzibar ili wananchi waweze kuelewa haki na wajibu wao.

45. **Mhe. Spika,** katika kipindi kifupi tangu kuimarishwa upya kwa Tume, sheria kumi na mbili zimefanyiwa mapitio kama ifuatavyo; Sheria ya Ushahidi sura ya 5/1917, Sheria ya Vileo sura ya 163, Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria namba 16/1986, Sheria ya Rasilimali Mifugo namba 11/1999, "The Legal Practitioners Decree" sura 28/1941,"The Notaries Public Decree" sura ya 29/1948, Sheria ya Usafirishaji Bidhaa kwa njia ya Bahari sura 155/1926, Sheria ya Ukomo sura ya 12/1917, Sheria ya Mikataba sura ya 149/1917"The Succession Decree" sura ya 21/1917, "The External Probates Decree" sura ya 22/1918, na "The Vagrancy Decree sura ya 21/1962".

46. **Mhe. Spika,** kwa mwaka 2014/15, Tume ilipanga kufanya mapitio ya sheria 4, ambazo ni "The Succession Decree" sura ya 21/1917, "The External Probates Decree" sura ya 22/1918, The Vagrancy Decree sura ya 21/1962 na Sheria ya Utalii kama ilivyorekebishwa na sheria namba 7/2012. Mpaka kufikia Machi, 2015 mapitio ya sheria tatu yamekamilika na mapitio ya Sheria ya Utalii yamesita kutokana na mabadiliko ya Sera ya Utalii yanayoendelea kufanywa chini ya uongozi wa wizara inayohusika.

47. **Mhe. Spika,** Tume imetayarisha na kurusha vipindi sita vya redio na vitatu vya televisheni ili kutoa elimu kwa umma kuhusu matumuzi ya Sheria za Zanzibar. Aidha, Tume imefanya Semina kuhusu mapitio ya Sheria kwa wadau mbalimbali wakiwemo Mahakimu, Mawakili wa kujitegemea, Wanasheria wa Serikali, Askari Polisi, Viongozi

wa Dini, Walimu, Wanafunzi, na Asasi za Kiraia zikiwemo Kituo cha Huduma za Sheria (ZLSC) na Wanasheria wa Chama cha Wanasheria Zanzibar (ZLS).

48. **Mhe. Spika,** katika kudumisha ushirikiano kitaifa na kimataifa, Tume inaendelea kuwa mwanachama wa Tume za Kurekebisha Sheria wa Afrika Mashariki, Kusini na Kati (ALRAESA) na Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria wa Jumuiya ya Madola (CALRAs). Vilevile, Tume imeendelea na ushirikiano na taasisi zilizo katika nchi mbalimbali kama vile Uganda, Uingereza na India, ili kubadilishana uzoefu kwa kushiriki katika mikutano yenye lengo la kuijengea Tume mustakbali mzuri kiutendaji.

49. **Mhe. Spika,** Tume ya Kurekebisha Sheria imewapatia mafunzo watendaji wake wanne katika kada tofauti kama ifuatavyo:- Wafanyakazi watatu walipata mafunzo mafupi ya miliki ubunifu (Intellectual Property Rights) nchini China, mfanyakazi mmoja anaendelea na mafunzo ya stashahada ya uhifadhi na uwekaji wa kumbukumbu, na wafanyakazi wanne wanatarajiwa kuhitimu mafunzo yao mwezi Julai 2015 katika kada ya sheria, uhasibu, kompyuta na ukatibu muhtasi.

50. **Mhe. Spika,** katika mwaka wa fedha 2014/15, Tume ya Kurekebisha Sheria iliidhinishiwa jumla ya shilingi 498,000,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 158,000,000.00 kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 340,000,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2015 shilingi 250,044,850.00 (50%) zilipatikana, zikiwemo shilingi 123,184,850.00 (78%) kwa ajili ya

mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 126,860,000.00 (37%) kwa matumizi mengineyo.

B6 AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

51. Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ina jukumu la usimamizi wa mashtaka ya jinai Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2014/15 afisi imeendelea kusimamia kesi za jinai na kutoa ushauri wa kisheria kwa Jeshi la Polisi na taasisi mbalimbali za serikali pamoja na raia. Katika kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015 jumla ya Kesi za Jinai 5,321 zimefunguliwa katika Mahkama mbalimbali Unguja na Pemba. Kati ya kesi hizo, kesi 4,312 zimeshatolewa uamuzi na kesi 1,009 zinaendelea katika hatua tofauti.

52. Mhe. Spika, katika mwaka 2014/15 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilipanga kuimarisha na kuendeleza uendeshaji wa Mashtaka Kiraia kwenye wilaya ambazo bado hazijafikiwa na huduma hiyo. Katika kutekeleza azma hiyo, Afisi imeajiri wanasheria wapya watano ili kufanya kazi katika mahkama mbalimbali za Unguja na Pemba. Aidha, Afisi imeendelea kutekeleza mpango wake wa kujenga nyumba za makaazi ya waendesha mashtaka huko Makunduchi, Mwera na Mkokotoni, ambapo kwa kipindi hiki Afisi imemaliza ujenzi wa nyumba iliyopo Madungu Chake chake Pemba.

53. Mhe. Spika, kazi ya uendeshaji wa mashtaka inahitaji mashirikiano baina ya taasisi zinazosimamia haki za jinai. Katika kutekeleza suala hilo, Afisi imefanikiwa kupunguza mwanya uliopo baina ya wadau kwa kujenga ukaribu kati ya Afisi na wadau wengine wa jinai ikiwemo Jeshi la Polisi, Mahkama, Mawakili wa Utetezi na jamii kwa ujumla. Afisi

imefanya mikutano kumi iliyohusisha Waendesha Mashtaka na Wapelelezi.

54. Mhe. Spika, katika jitihada za kuendeleza taaluma zinazohusu uwanja wa sheria, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kupitia Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria, inaendelea kutoa mafunzo ya Usimamizi wa Sheria kwa watendaji mbalimbali wa Serikali na taasisi binafsi wakiwemo wanasheria. Miongoni mwa mafunzo yaliyotolewa ni uandishi wa sheria (Legislative Drafting) na usimamizi wa sheria ya wafanyakazi wa umma (Public Service Law Training). Katika kipindi cha mwaka 2014/15, Kituo kimefanikiwa kutoa mafunzo ya stashahada ya sheria pamoja na cheti.

55. Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeendelea na hatua ya kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya haki za jinai kwa kurusha hewani vipindi vya redio na televisheni. Katika kukuza uwezo wa Afisi kiutendaji, jumla ya wafanyakazi 14 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika nyanja mbalimbali zikiwemo sheria, utawala na maktaba. Kati ya hao wanaume ni wanane na wanawake ni sita. Jumla ya wanasheria kumi walihudhuria warsha mbalimbali za mafunzo ya muda mfupi ambayo yamewaongezea ujuzi wa kutekeleza majukumu ya kazi.

56. Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,288,500,000.00 kwa kazi za kawaida, ambapo shilingi 871,900,000.00 ni kwa malipo ya mishahara na stahiki za wafanyakazi na shilingi 416,600,000.00 kwa matumizi mengineyo. Afisi pia iliidhinishiwa shilingi 200,000,000.00

kwa kazi za maendeleo na shilingi 77,500,000.00 za ruzuku. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2015, fedha zilizopatikana kwa kazi za kawaida ni shilingi 1,071,016,950.00 (83%). Kati ya fedha hizo, shilingi 714,666,950.00 (82%) ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 356,350,000.00 (86%) kwa matumizi mengineyo. Shilingi 50,000,000.00 (25%) na shilingi 37,500,000.00 (48%) za ruzuku zimepatikana. (Kiambatanisho nam. 1 kinahusika).

57. Mhe. Spika, kwa mwaka 2014/15, Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti kilijipangia kukusanya shilingi 80,000,000.00. Hadi kufikia Machi 2015, kituo hicho kimekusanya jumla ya shilingi 42,371,500.00 sawa na (53%), na kwa mwaka 2015/16 kinatarajia kukusanya shilingi 80,000,000.00.

B7 AFISI YA MUFTI

58. Mhe. Spika, Afisi ya Mufti wa Zanzibar ina dhamana kisheria ya kuratibu na kusimamia shughuli za Kiislamu, ikiwemo kutoa fatwa na kusimamia miongozo kuhusu masuala ya kidini.

59. Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/15, Afisi ya Mufti imetekeleza malengo yake kwa kufanya Mikutano ya Baraza la Ulamaa, kuratibu na kusimamia Kamati ya Kitaifa ya kuthibitisha kuandama kwa Mwezi, kufanya ziara za misikiti na vyuo vya Qur-ani, kujibu maswali ya wananchi, kutatua migogoro ya kidini pamoja na kuhamasisha amani na utulivu.

60. Mhe. Spika, katika juhudi za kupata takwimu sahihi za misikiti na vyuo vya Qur-ani, Afisi ya Mufti imeweka utaratibu wa kugawa fomu kwa Masheha kupitia kwa Wakuu wa Wilaya ili wazijaze. Jumla ya fomu 215 za misikiti na 215 za madrasa zimesambazwa na fomu 159 za misikiti na madrasa zimerejeshwa. Kupitia fomu hizo jumla ya misikiti 1,018 na madrasa 1,097 vimetambuliwa kuwepo kwake katika shehia za Unguja. Vilevile Afisi ya Mufti imethibitisha usajili wa Misikiti 43 na Vyuo 56.

61. Mhe. Spika, kwa upande mwengine, jumla ya vyuo vya Qur-ani 46 na misikiti 39 vimetembelewa Unguja na Pemba, kwa lengo la kushauriana juu ya maendeleo ya taasisi hizo. Aidha, Afisi imepokea migogoro minane ya misikiti na mmoja wa Madrasa. Kati ya migogoro hiyo, saba imetatuliwa. Aidha, migogoro ya ndoa 83 imepokelewa na kupatiwa ufumbuzi.

62. Mhe. Spika, Afisi ya Mufti imeendelea kutoa elimu kwa umma. Jumla ya masuala 152 yanayohusiana na ndoa, talaka, pamoja na mirathi yamejibiwa na vipindi 72 vya masuala na majibu vimerushwa kupitia ZBC Redio. Pamoja na vipindi hivyo, Afisi imetoa nasaha na mawaidha yanayohusu maadili mema, kudumisha amani na utulivu, uongozi misikitini na umuhimu wa kushukuru neema za Mwenyeezi Mungu.

63. Mhe. Spika, Baraza la Ulamaa ni chombo chenye jukumu la kumsaidia Mheshimiwa Mufti kutoa fatwa. Kwa kipindi cha Julai - Machi 2014/15, Baraza hilo limekutana mara mbili na ajenda mbalimbali zilijadiliwa. Aidha, Kamati ya Kitaifa ya Kuthibitisha Kuandama kwa Mwezi imefanya vikao viwili na kutoa taarifa kwa wakati.

64. Mhe. Spika, Afisi ya Mufti kwa kushirikiana na Kamati ya Zafa ya Kitaifa iliandaa matembezi rasmi ya kidini (zafa) ya kuukaribisha mwaka mpya wa Kiislamu 1436 Hijria na kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (S.A.W). Sherehe hizo ziliwashirikisha walimu na wanafunzi wa vyuo vya Qur-ani, Viongozi wa dini ya Kiislamu, pamoja na waumini kutoka maeneo mbalimbali.

65. Mhe. Spika, mashirikiano mema na taasisi nyenginezo za kidini ndani na nje ya nchi hukuza udugu kwa waumini. Afisi ya Mufti kwa kushirikiana na Kamati ya Amani na Utulivu pamoja na Taasisi ya Friends of Zanzibar imefanya mikutano miwili Unguja na Mkutano mmoja Pemba. Mikutano hiyo ililenga kusisitiza kuwepo umoja, mshikamano, amani na utulivu katika nchi yetu. Aidha, Afisi imehudhuria mkutano nchini Uturuki na imefanya ziara ya kikazi katika visiwa vya Comoro. Vilevile, Afisi imepokea wageni kutoka International Islamic Relief Organisation (IIRO), Jumuiya ya Ulaya, UNDP, Global Peace Foundation, Anti Tribalism Movement, Uganda, India, Pakistan, Misri, Saudia Arabia, Iran na Algeria. Afisi pia imepokea mabalozi wa Amerika, Uingereza, Ujerumani na Ireland ya Kaskazini waliopo nchini Tanzania kwa lengo la kushauriana njia bora za kudumisha amani na utulivu nchini.

66. Mhe. Spika, katika kujenga uwezo, Afisi imewapeleka masomoni wafanyakazi wawili kwa ngazi ya shahada na wawili katika ngazi ya stashahada kwa Unguja na Pemba. Sambamba na hilo Afisi inaendelea na uimarishaji wa Maktaba ya Kiislamu, kwa kununua makabati ya kuwekea vitabu na kutafuta vitabu vyengine muhimu kwa ajili ya maktaba hiyo.

67. Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Afisi ya Mufti iliidhinishiwa jumla ya shilingi 500,610,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 367,544,000.00 zilitengwa kwa malipo ya mishahara na stahiki nyengine za watumishi, na shilingi 133,066,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2015, fedha zilizopatikana ni shilingi 306,193,489.00 sawa na asilimia (61%). Kati ya fedha hizo shilingi 232,985,625.00 sawa na asilimia (63%) zilitumika kwa kulipa mishahara na stahiki, na shilingi 73,207,864.00 sawa na asilimia (55%) kwa matumizi mengineyo (Kiambatanisho Nam.1 kinahusika).

B8 WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI

68. Mhe. Spika, Afisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali 'Business and Property Registration Agency' (BPRA) ina jukumu la kufanya usajili wa biashara, hati za mali za ubunifu, pamoja na usajili wa nyaraka mbalimbali zinazowahusu wananchi na wageni wanaofanya shughuli zao Zanzibar.

69. Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:- Kuimarisha mazingira ya kazi kwa ajili ya kutoa huduma bora; kuandaa kanuni za sheria za Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali; kufanya Usajili wa Taasisi za Biashara na Usajili wa Dhamana za Mali zinazohamishika; na kuendelea na uwekaji wa mifumo ya kisasa ya usajili.

70. Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai - Machi 2014/15 Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali imesajili Kampuni 202, Majina ya Biashara 618, Alama za Biashara 719, Nyaraka 819 na Jumuiya za Kiraia 63.

71. Mhe. Spika, kwa kuzingatia mabadiliko mbalimbali yanayotokea ulimwenguni, BPRA inaendelea kuimarisha miundombinu ya usajili ili kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. Vilevile, Afisi inaendelea na kazi ya kukamilisha sera ya mali za ubunifu kwa kushirikiana na WIPO. Aidha, BPRA imetengeneza rasimu za kanuni za Sheria ya Wakala wa Usajili Biashara na Mali Zanzibar na kanuni za Sheria ya Usajili wa Taasisi za Biashara pamoja na kuandaa muongozo wa usajili wa biashara Zanzibar 'Business Registration Manual'.

72. Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi wake, BPRA inaendelea kusomesha wafanyakazi watatu katika ngazi ya shahada ya sheria, stashahada ya ugavi na manunuzi, na shahada ya takwimu. Aidha wafanyakazi wanne wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya huduma kwa wateja na uhifadhi kumbukumbu kwa kutumia kompyuta "Electronic Document Management System".

73. Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, BPRA iliidhinishiwa jumla ya shilingi 313,267,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 170,189,000.00 zilitengwa kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 143,078,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2015 fedha zilizopatikana ni shilingi 180,058,519.00 (57%). Kati ya fedha hizo, shilingi 127,634,400.00 (75%) zilitumika kulipa mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 52,424,119.00 (37%) kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2015, Wakala ilipata shilingi 15,000,000.00 kutoka Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa ajili ya kazi za maendeleo. Vilevile, Afisi ilikadiriwa kukusanya shilingi 126,494,000.00. Hadi kufikia Machi 2015, shilingi

107,139,150.00 (85%) zilikusanywa (Viambatanisho nam. 1,3&4 vinahusika).

B9 AFISI YA MRAJIS WA VIZAZI NA VIFO

74. **Mhe. Spika,** Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo ina dhima kisheria ya kusajili vizazi na vifo pamoja na kutunza kumbukumbu zinazotokana na usajili huo. Afisi hii pia inawajibika kuishauri Serikali kuhusu masuala ya usajili wa vizazi na vifo, kutoa mafunzo yanayohusiana na usajili kwa watendaji na wakala wa usajili pamoja na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya usajili wa vizazi na vifo.

75. **Mhe. Spika,** kwa mwaka 2014/15, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo imesajili vizazi 43,501. Kati ya hao wanawake ni 21,418 na wanaume ni 22,083. Pia Afisi imesajili vifo 2,425; wakiwemo wanaume 1,327 na wanawake 1,098. Kutokana na takwimu hizo ni wazi kwamba uandikishwaji wa vifo ni mdogo. Hali hiyo inatokana na mwamko mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa kufanya usajili wa vifo. Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo inaendelea na utaratibu wa kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa usajili wa vizazi na vifo. Ninachukua fursa hii pia kuwashauri Wajumbe wa Baraza lako tukufu kusaidia kuendeleza juhudi za kuelimisha wananchi katika maeneo yao.

76. **Mhe. Spika,** Afisi pia inaendelea na marekebisho ya mfumo wa usajili ili kuelekea kwenye usajili na uhifadhi kumbukumbu unaotumia kompyuta. Katika kutekeleza hilo, Afisi ilifanya majaribio ya mfumo huo katika Wilaya ya Magharibi Unguja na kuweza kugundua kasoro ambazo tayari imechukua hatua za kuzirekebisha. Kazi hiyo ya

marekebisho inafanywa kupitia mkataba uliosainiwa na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar na wataalamu elekezi waliounda mfumo huo kutoka Norway. Sambamba na kazi hiyo, Afisi inafanya jitihada za kuingiza taarifa za miaka ya nyuma kwenye kompyuta, kutoa mafunzo kwa mawakala wa usajili na kuihamasisha jamii kupitia vyombo vya habari. Mabadiliko haya yatakapokamilika yatasaidia upatikanaji wa kumbukumbu na vyeti kwa njia rahisi na ya haraka. Katika hatua za kuziandaa afisi za usajili wilayani ili kuupokea mfumo mpya wa usajili, Afisi imekamilisha ukarabati wa Afisi za Chakechake na Mkoani pamoja na kujenga upya Afisi ya Micheweni. Aidha Afisi pia imefunga makabati ya kutunzia kumbukumbu na kuweka samani mpya katika Afisi hizo.

77. **Mhe. Spika,** katika kujenga uwezo kiutendaji, Afisi imeendelea kumpatia mfanyakazi mmoja mafunzo ya stashahada ya utunzaji na uhifadhi wa nyaraka na watumishi wawili wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya huduma kwa wateja. Aidha Afisi imeendelea kushiriki kikamilifu katika kikao cha pamoja cha wadau wa taasisi za usajili zinazojumuisha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Uhamiaji, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum, Afisi ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar. Kikao hicho hufanyika kila baada ya miezi mitatu kwa lengo la kujadili changamoto, mafanikio na ushirikiano unaohitajika ili kuongeza ufanisi katika usajili na utambulisho.

78. **Mhe. Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo iliidhinishiwa jumla ya shilingi 418,083,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi

232,923,000.00 zilitengwa kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 185,360,000.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2015, fedha zilizopatikana ni 178,862,553.00 (43%) kwa kazi za kawaida, ambapo shilingi 122,606,500.00 (53%) ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 56,256,053.00 (30%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, jumla ya shilingi 50,000,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo kutoka Serikalini na zilizopatikana ni shilingi 15,000,000.00 (30%). Afisi pia ilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi 221,000,000.00. Kufikia Machi 2015, jumla ya shilingi 153,911,435.00 (70%) zilikusanywa (Viambatanisho nam. 1,3&4 vinahusika).

B10 AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI

79. Mhe. Spika, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki ina jukumu la kusimamia matumizi halali ya hakimiliki ili kuhakikisha hali, hadhi na maslahi ya wabunifu na wasanii vinaimarika. Katika kutekeleza jukumu hilo, Afisi inakusanya mirabaha kutoka kwa watumiaji wa kazi hizo kibiashara na kuigawa kwa wabunifu na wasanii waliojisajili.

80. Mhe. Spika, hivi karibuni Afisi imefanya mgawo wa fedha za mirabaha zinazokusanywa kutokana na matumizi ya kazi za sanaa na ubunifu. Katika mgawo huo, jumla ya shilingi 41, 876,881.00 za mirabaha ziligaiwa kwa wabunifu na wasanii wapatao 1,124. Mbunifu aliyepata kiwango cha juu zaidi alipata shilingi 575,500.00 na kiwango cha chini kilikuwa shilingi 13,000.00.

81. Mhe. Spika, Afisi inaendelea kukabiliana na changamoto za ulipaji wa mirabaha hasa kwa vituo binafsi vya utangazaji. Afisi inatoa elimu kwa wasanii, wabunifu, watumiaji wa kazi na jamii kwa jumla ili dhana ya usimamizi wa pamoja iweze kufikiwa. Aidha, Afisi imeshirikiana na Kamisheni ya Utalii kufanya mazungumzo na watumiaji wa kazi za hakimiliki ili waweze kulipia mirabaha ambapo Hoteli 84 zilifikiwa. Kati ya hoteli hizo, ni hoteli tisa tu ndizo zilifanya malipo. Kwa upande wa vituo vya utangazaji, Zanzibar Cable Televisheni walifanya malipo na Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) lilipunguza kiasi cha deni linalodaiwa. Nachukua fursa hii kuwaomba ZBC kulipa deni lililobakia ili kwa pamoja tuchangie kulinda haki za wabunifu wetu. Afisi imejipanga kuimarisha mashirikiano na Tume ya Utangazaji ya Zanzibar, ili iweze kupata taarifa za awali za vituo vya utangazaji vinavyoomba leseni ya kurusha matangazo yao hapa Zanzibar. Lengo la ushirikiano huu ni kuiwezesha Afisi ya Hakimiliki kuwaelimisha wamiliki hao juu ya kufanya matumizi halali ya hakimiliki katika vituo vyao.

82. Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai- Machi, 2014/2015, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki imeingiza taarifa za kazi za usajili na uhifadhi wa kumbukumbu katika mfumo wa WIPOCOS (WIPO Software for Collective Management Organization), ambapo jumla ya kazi 138 za hakimiliki zimesajiliwa (Kiambatanisho Nam. 8 kinahusika).

83. Mhe. Spika, nchi yetu inakabiliwa na changamoto ya picha chafu. Afisi imeligundua hili wakati wa operesheni zake za kawaida za kupunguza uharamia wa hakimiliki. Jukumu la kupambana na suala hili ni la taasisi zinazosimamia mila na

utamaduni, vyombo vya ulinzi na jamii kwa ujumla. Nazipa hamasa taasisi hizo zishirikiane nasi, ili kwa pamoja tuweze kulidhibiti suala hili.

84. **Mhe. Spika,** Afisi kwa kushirikiana na Shirika la Mali Ubunifu Ulimwenguni (WIPO) ilifanya mikutano miwili juu ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki (Nam. 14) ya mwaka 2003 kwa wadau wakiwemo wasimamizi wa Sheria na baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa upande mwingine, Afisi imeendelea kualikwa kutoa mihadhara katika Chuo Kikuu cha Zanzibar katika somo la Ujasiriamali na Miliki Ubunifu. Katika kujiimarisha kiutendaji, Afisi imewapatia wafanyakazi watatu mafunzo ya muda mfupi juu ya usimamizi wa hakimiliki.

85. **Mhe. Spika,** katika mwaka wa fedha 2014/15, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki iliidhinishiwa ruzuku ya shilingi 170, 000,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 85, 647,600.00 zilitengwa kulipia mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 84,352,400.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2015, fedha zilizopatikana ni shilingi 105,575,430.00 (62%), ambapo kati ya hizo shilingi 63,139,400.00 (74%) zilipatikana kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 42, 436,030.00 (50%) kwa matumizi mengineyo (Kiambatanisho nam. 1 kinahusika).

B11 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

86. **Mhe. Spika,** jukumu la Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ni kusimamia mali za wakfu, mali za amana, mirathi ya waislamu, sala na mabaraza ya Iddi kitaifa, Hijja, zakka, sadaka na misaada ya kheri.

87. Mhe. Spika, Kamisheni imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kawaida, ikiwemo kukusanya na kugawa zakka, sadaka na misaada ya kheri. Kwa kipindi cha Julai - Machi 2014/2015, misaada ya kheri yenye thamani ya shilingi 573,646,000.00 imekusanywa. Kati ya missada hiyo, misaada yenye thamani ya shilingi 299,372,000.00 imegawiwa kwa wanufaika mbalimbali. Aidha, Kamisheni imetembelea na kufanya vikao 26 vya kuelimisha na kuhamasisha wanufaika wa mali hizo kuzitunza. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, imeendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za kidini kufanikisha upatikanaji wa misaada ya kheri. Miongoni mwa misaada iliyopokelewa ni nyama ya kondoo, nyama ya mbuzi, tende na nguo.

88. Mhe. Spika, Kamisheni imeendelea kutoa taaluma kuhusu Wakfu na Amana. vipindi viwili vya Zanzibar Cable Television (ZCTV), vinne vya ZBCTV na 14 vya ZBC Radio vimerushwa hewani. Mikutano mitano ya wadau imefanywa ikijumuisha minne kwa wilaya za Pemba na mmoja kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Vitabu 57 vya mwongozo wa Wakfu na mwongozo wa Zakka vimegaiwa. Aidha, kazi ya utafiti wa kuzitambua mali za wakfu, kutafuta nyaraka zilizopotea, kujua wasia wa wakfu hizo pamoja na kuwatambua wanufaika halali imeendelea. Kwa mujibu wa utafiti huo, nyakfu mpya 14 zimepatikana na kusajiliwa.

89. Mhe. Spika, katika kusimamia mirathi, Kamisheni imefungua mafaili 905 ya mirathi na mafaili 413 yenye thamani ya shilingi 6,037,171,495.00 yamefungwa na warathi kupatiwa haki zao. Katika kurithisha hujitokeza mizozo ambayo hulazimu kutafutiwa ufumbuzi. Katika kipindi

cha Julai hadi Machi 2014/15 mizozo 86 imeshughulikiwa, kati ya hiyo mizozo 15 imepatiwa ufumbuzi, mizozo kumi inaendelea na jumla ya kesi 61 zimesimamiwa mahakamani.

90. Mhe. Spika, Kamisheni imeendelea kuwawekea mazingira mazuri wapangaji wa nyumba za wakfu ili waweze kulipa kodi vizuri na wanufaika waweze kufaidika na mali zilizowekwa wakfu. katika kipindi hiki, kodi zenye thamani ya shilingi 246,628,342.00 za nyumba za wakfu, shilingi 2,195,000.00 za mashamba na shilingi 42, 905,060.00 za nyumba za amana zimekusanywa Unguja na Pemba. Fedha hizo tayari zimegawiwa kwa wanufaika. Aidha, Kamisheni imezikagua nyumba 153 na msikiti mmoja. Matokeo ya ukaguzi huo yalionesha kwamba nyumba 22 zilikuwa zinahitaji matengenezo ya haraka yaliyogharimu shilingi 93, 653,980.00.

91. Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana pia ina jukumu la kusimamia Sala na Mabaraza ya Iddi Kitaifa. Kwa mwaka wa fedha 2014/15 sala na mabaraza ya Iddi kitaifa yaliratibiwa vyema na kufanyika kwa ufanisi. Sala ya Iddi El Fitri ilisaliwa kwenye Viwanja vya Maisara na Baraza la Idd lilifanyika katika Ukumbi wa Salama Hoteli ya Bwawani, wakati sala ya Iddi el Hajj ilisaliwa Konde na Baraza la Idd lilifanyika Chuo cha Kiislamu Micheweni Pemba.

92. Mhe. Spika, Kamisheni imeendelea na kazi ya kusimamia safari za Hija kama ilivyo kawaida, jumla ya mahujaji 1,086 walisafirishwa na vikundi tisa vya Zanzibar. Vikundi vipya vitano vimeruhusiwa kusafirisha mahujaji katika kipindi hiki. Aidha, katika kufanikisha kazi hiyo, Kamisheni

imeelimisha jamii na wadau wa Hijja kwa kurusha hewani kipindi, kufanya vikao vinane na kuandaa makala katika gazeti (Kiambatisho nam. 7 kinahusika).

93. Mhe. Spika, Kamisheni imeanzisha na kuendeleza mahusiano na mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi kwa maslahi ya taifa. Aidha, mkutano mmoja wa majadiliano na taasisi ya "World Monument Fund" kuhusiana na udhamini wa mafunzo ya urithi wa dunia (World Heritage) ulifanyika na hivi sasa watendaji wetu wawili wanahudhuria mafunzo ya miezi saba katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

94. Mhe. Spika, katika kuimarisha ofisi kiutendaji wafanyakazi kumi wamelipiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Vilevile jumla ya Wafanyakazi 19 wamepatiwa mafunzo ya ndani ya Kanuni za Utumishi 2014 na sheria ya mirathi.

95. Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/15 Kamisheni iliidhinishiwa ruzuku ya shilingi 517,800,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 378,634,000.00 zilitengwa kulipia mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 139,166,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2015 fedha zilizoingizwa ni shilingi 399,465,181.00 (77%). Kati ya fedha hizo, shilingi 265,329,266.00 (70%) zilitumika kwa malipo ya mishahara na stahiki za wafanyakazi na shilingi 134,135,915.00 (96%) zilitumika kwa matumizi mengineyo (Kiambatanisho nam. 1 kinahusika).

B12 AFISI KUU PEMBA

96. Mhe. Spika, Afisi Kuu Pemba ni mhimili mkuu katika kusimamia shughuli za utendaji wa wizara pamoja na taasisi

zake kisiwani Pemba. Katika kipindi cha mwaka 2014/15, Afisi Kuu Pemba imetekeleza majukumu yake ya kusimamia shughuli za wizara kama ifuatavyo:-

97. Mhe. Spika, Afisi imeendelea kuratibu masuala ya Idara zilizopo chini ya wizara kwa upande wa Pemba kwa lengo la kuzidisha uwajibikaji. Vilevile, Afisi imefanya mikutano miwili ya robo mwaka kwa watendaji wakuu wa idara za wizara zilizoko Pemba. Mbali ya majukumu hayo, Afisi Kuu Pemba pia imeshiriki vikao vya wizara vinavyohusu utekelezaji wa majukumu ya wizara, imetoa mwongozo kuhusu utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu za wafanyakazi na imetayarisha Nominal Roll.

98. Mhe. Spika, miongoni mwa kazi za Afisi Kuu Pemba ni kuratibu shughuli za Jumuiya zisizo za Kiserikali (NGOs). Afisi kupitia kitengo cha jumuiya za kiraia imezikagua baadhi ya jumuiya ili kuona maendeleo ya jumuiya hizo. Aidha, Afisi imekutana na viongozi wa jumuiya hizo kwa lengo la kutathimini utendaji na kuhamasisha matumizi mazuri ya fedha wanazozipata katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

99. Mhe. Spika, katika kuwajengea uwezo watendaji, Afisi imewasomesha wafanyakazi watano, wakiwemo wanawake wawili na wanaume watatu katika ngazi ya shahada ya pili, shahada ya kwanza na cheti. Aidha, Afisi Kuu Pemba imelifanyia matengenezo madogo jengo lake na kununua vifaa vya kufanyia kazi.

100. Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15 Afisi Kuu Pemba ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 249,291,000.00 kwa kazi

za kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 157,792,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 91,499,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2015, jumla ya shilingi 154,342,310.00 zimepatikana (62%), ambapo shilingi 117,212,000.00 (74%) ni kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 37,130,310.00 (41%) kwa matumizi mengineyo.

C. MWELEKEO WA MATUMIZI YA BAJETI INAYOTUMIA PROGRAMU

101. Mhe. Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inasimamia Mafungu matano ambayo ni Fungu la Wizara (G01), Fungu la Mahkama (G02), Fungu la Afisi ya Mwanasheria Mkuu (G03), Fungu la Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (G04) na Fungu la Tume ya Kurekebisha Sheria (G05). Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Katiba na Sheria itatumia jumla ya shilingi 14,216,700,000.00 kwa ajili ya kutekeleza programu zilizobainishwa katika mafungu haya. Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa uniruhusu nizichambue programu zinazotarajiwa kutekelezwa na Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

Fungu G01 - Wizara ya Katiba na Sheria

102. Mhe. Spika, Fungu la Wizara linazo Programu mbili ambazo ni Programu ya Usajili na Usimamizi wa Masuala ya Dini na Programu ya Uendeshaji wa Sekta ya Sheria. Programu ya Usajili na Usimamizi wa Masuala ya Dini imegawika katika Programu Ndogo nne ambazo ni Usajili wa Matukio ya kijamii, Usajili wa Biashara na Mali, Usimamizi wa Hakimiliki na Usimamizi wa masuala ya dini. Matokeo

yanayokusudiwa kufikiwa katika utekelezaji wa programu hii ni kuimarika kwa mifumo ya usajili wa matukio ya kijamii, biashara na mali, usimamizi wa hakimiliki na usimamizi masuala ya dini ili kuongeza ufanisi.

103. Mhe. Spika, Programu ya Uendeshaji wa Sekta ya Sheria imegawika katika programu ndogo tatu ambazo ni Uongozi na Uendeshaji, Mipango, Sera na Utafiti, na Uratibu na Uendeshaji wa Sekta ya Sheria Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Fungu G01 limepangiwa kutumia shilingi 5,909,300,000.00 na fedha hizi zitasimamiwa na Katibu Mkuu. Ufafanuzi zaidi unapatikana katika Kitabu cha Bajeti ya Serikali.

Fungu G02 - Mahkama

104. Mhe. Spika, Fungu G02 linahusu Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki. Jukumu la Programu hii ni kuhakikisha kuwa haki inasimamiwa vyema na inapatikana kwa wakati. Matokeo yanayotarajiwa katika kutekeleza programu hii ni kupungua kwa muda wa usikilizaji mashauri na utoaji hukumu katika ngazi mbalimbali za Mahkama ili kufikia upatikanaji wa haki. Fungu G02 linasimamia pia Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Uendeshaji na Utawala wa Mahkama. Matokeo yanayotarajiwa katika kutekeleza programu hii ni kuimarika kwa utekelezaji wa kazi za uendeshaji shughuli za mahkama. Fungu G02 limepangiwa kutumia jumla ya shilingi 5,143,100,000.00 na linasimamiwa na Mrajis wa Mahkama.

Fungu G03 – Mwanasheria Mkuu wa Serikali

105. **Mhe. Spika, Fungu G03 linahusu Programu ya Utoaji Huduma za Kisheria ambayo jukumu lake ni kushauri na kusimamia** masuala yote ya kisheria yakiwemo mashauri ya madai yanayoihusu serikali, uandaaji wa mikataba ya kitaifa na kimataifa, miswada ya sheria, na hati na nyaraka za kisheria. Matokeo ya programu hii ni kuimarika kwa huduma za Kisheria. Fungu G03 pia linahusu Programu ya Uendeshaji wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Matokeo yanayotarajiwa katika kutekeleza programu hii ni kuimarika kwa utekelezaji wa kazi za uendeshaji za Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Fungu G03 limepangiwa kutumia jumla ya shilingi 1,010,200,000.00 na linasimamiwa na Mwanasheria Mkuu.

Fungu G04 – Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

106. **Mhe. Spika,** Fungu G04 linahusu Programu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Jinai ambayo inahusu usimamizi wa mashtaka ya jinai. Matokeo ya programu hii ni kupatikana kwa haki za jinai ili kuimarisha amani, utulivu na maendeleo ya kiuchumi. Programu hii pia inahusika na kutoa ushauri wa kisheria juu ya haki za jinai na kuratibu shughuli za uendeshaji wa mashtaka. Aidha, Programu ya Mipango na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inatekelezwa chini ya Fungu G04. Mbali na shughuli za mipango na uendeshaji, programu hii inahusu utekelezaji shughuli za uendeshaji mashtaka Pemba. Fungu G04 limetengewa jumla ya shilingi 1,627,100,000.00 na litasimamiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

Fungu G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria

121. **Mhe. Spika,** Fungu G05 linahusu Programu ya Mapitio ya Sheria za Zanzibar na kupendekeza marekebisho yake kwa lengo la kuzifanya sheria hizo ziende sambamba na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Mapitio hayo yanahusisha ushiriki wa wananchi na wadau wa sheria ambao ndio watumiaji wa sheria hizo. Matokeo ya utekelezaji wa programu hii ni kuwepo kwa sheria zinazokwenda na wakati kulingana na mazingira ya sasa. Programu nyengine inayotekelezwa chini ya Fungu G05 inahusu Uendeshaji na Utawala wa Afisi ya Tume ya Kurekebisha Sheria na lengo lake ni kuimarisha utendaji kazi za kila siku za Tume. Fungu hili limepangiwa kutumia shilingi 527,000,000.00 na linasimamiwa na Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria.

D. SHUKURANI

122. **Mhe. Spika,** baada ya kutoa maelezo hayo, natoa shukrani nyingi sana kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuweza kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu. Naomba pia niwashukuru kwa dhati wadau na washirika mbalimbali wa maendeleo kwa ushirikiano mzuri walioutoa kwa Wizara ya Katiba na Sheria na kurahisisha utekelezaji wa shughuli zake. Miongoni mwao ni:- UNDP, Jumuiya ya Ulaya (EU), UNICEF, UNFPA, Shirika la Kimataifa la Mali za Ubunifu (WIPO), Shirika la Mali Bunifu la Afrika (ARIPO), Benki ya Dunia, African Muslim Agency, Benki ya Maendeleo ya Kiislam (IDB), na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Tunawashukuru pia Save the Children, Wizara za Wakfu za Oman na Qatar, Taasisi ya Al-Rahma ya Falme za Kiarabu (UAE) na Shirika la Dan Mission la

Denmark. Wizara ya Katiba na Sheria inazishukuru nchi ya Saudi Arabia, Oman, na Egypt; na Taasisi za nchi ya Uturuki zikiwemo The Humanitarian Aid Foundation (IHH), Turkey Cooperation and Coordination Agency (TIKA), Turkey Dianet Vakfi na Turkey Directorate of Foundation. Wizara inatoa shukrani kwa Vyombo vya Sheria vya Jamhuri ya Muungano zikiwemo Mahkama, Tume ya Kurekebisha Sheria, Afisi ya Mwanasheria Mkuu, na Jeshi la Polisi. Vilevile, tunatoa shukrani kwa Chama cha Wanasheria Zanzibar (ZLS), Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC), na Chama cha Wanasheria Wanawake (ZAFELA); Vikundi vilivyosafirisha Mahujaji, Jumuiya na Taasisi mbalimbali za kidini; wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Masheha na wananchi wote kwa jumla.

123. **Mhe. Spika,** vilevile, kwa ujumla naomba niwashukuru wote walioisaidia Wizara ya Katiba na Sheria katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, ninawashukuru Watendaji Wakuu na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano nilioupata kutoka kwao katika kipindi chote tulicho kuwa pamoja. Aidha, naomba kuwaambia washirika wetu kwamba wizara itaendelea kuthamini sana michango yao ya hali na mali pamoja na ushirikiano wanaotupatia kila tulipokuwa tukiwahitaji. Ninachoweza kusema kwao ni ahsanteni na tunawathamini sana na kushukuru kwa yote. Kwa niaba ya Wizara ya Katiba na Sheria na serikali kwa jumla tunaomba mzipokee shukurani zetu, ahsanteni na Mungu awabariki.

E. HITIMISHO

124. Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kukumbusha kuwa Sekta ya Katiba na Sheria inayo dhima ya kuhakikisha kuwa masuala yanayohusu haki za wananchi na wageni wanaofanya shughuli zao hapa Zanzibar zinalindwa kupitia vyombo vyake vya sheria, dini pamoja na usajili. Utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko Katika Sekta ya Sheria unalenga kuongeza ushiriki wa wananchi katika masuala ya kisheria. Ili Wizara ya Katiba na Sheria iweze kutekeleza programu zake vyema, naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu wachangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waidhinishe jumla ya shilingi 14,216,700,000.00 kwa matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha wa 2015/16. Naomba pia Baraza lako liikubalie wizara ichangie shilingi 725,064,000.00 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali (Viambatanisho Nam 2,3 & 4 vinahusika).

125. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2014/15

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI ILIOTENGWA	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI-MACHI	ASILIMIA (%)
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	Mishahara na Stahiki	128,784,000	84,923,500	66%
	Matumizi Mengineyo	95,468,000	24,644,050	26%
	Jumla	**224,252,000**	**109,567,550**	**49%**
	Maendeleo Serikali	150,000,000	50,000,000	33%
	Maendeleo - UNDP	1,579,748,700	630,530,050	40%
	Jumla	**1,729,748,700**	**680,530,050**	**39%**
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Mishahara na Stahiki	465,723,000	287,680,750	62%
	Matumizi Mengineyo	250,438,000	104,594,250	42%
	Jumla	**716,161,000**	**392,275,000**	**55%**
Mahkama	Mishahara na Stahiki	3,536,700,000	2,739,663,400	77%
	Matumizi Mengineyo	1,500,000,000	585,702,805	39%
	Jumla	**5,036,700,000**	**3,325,366,205**	**66%**
	Maendeleo Serikali	700,000,000	200,000,000	29%
	Makusanyo	95,000,000	128,346,107	135%
	Jumla Kuu	**5,831,700,000**	**3,653,712,312**	**63%**
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	Mishahara na Stahiki	461,900,000	311,192,025	67%

Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2014/15

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI ILIOTENGWA	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI-MACHI	ASILIMIA (%)
Tume ya Kurekebisha Sheria	Matumizi Mengineyo	537,400,000	310,157,550	58%
	Jumla	**999,300,000**	**621,349,575**	**62%**
	Mishahara na Stahiki	158,000,000	123,184,850	78%
	Matumizi Mengineyo	340,000,000	126,860,000	37%
	Jumla	**498,000,000**	**250,044,850**	**50%**
Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka				
	Mishahara na Stahiki	871,900,000	714,666,950	82%
	Matumizi Mengineyo	416,600,000	356,350,000	86%
	Jumla	**1,288,500,000**	**1,071,016,950**	**83%**
	Maendeleo Serikali	200,000,000	50,000,000	25%
	Ruzuku	77,500,000	37,500,000	48%
	Makusanyo	80,000,000	42,371,500	53%
	Jumla Kuu	**1,566,000,000**	**1,158,516,950**	**74%**

Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2014/15

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI ILIOTENGWA	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI-MACHI	ASILIMIA (%)
Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali	Mishahara na Stahiki	170,189,000	127,634,400	75%
	Matumizi Mengineyo	143,078,000	52,424,119	37%
	Jumla	**313,267,000**	**180,058,519**	**57%**
	Makusanyo	126,494,000	107,139,150	85%
Afisi ya Vizazi na Vifo	Mishahara na Stahiki	232,923,000	122,606,500	53%
	Matumizi Mengineyo	185,160,000	56,256,053	30%
	Jumla	**418,083,000**	**178,862,553**	**43%**
	Makusanyo	221,000,000	153,911,435	70%
	Maendeleo Serikali	50,000,000	15,000,000	30%
	Jumla	**271,000,000**	**168,911,435**	**62%**
	Jumla Kuu	**689,083,000**	**347,773,988**	**50%**
Afisi ya Mufti wa Zanzibar	Mishahara na stahiki	367,544,000	232,985,625	63%
	Matumizi Mengineyo	133,066,000	73,207,864	55%
	Jumla	**500,610,000**	**306,193,489**	**61%**

Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2014/15

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI ILIOTENGWA	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI-MACHI	ASILIMIA (%)
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	Mishahara na Stahiki	378,634,000	265,329,266	70%
	Matumizi Mengineyo	139,166,000	134,135,915	96%
	Jumla ruzuku	**517,800,000**	**399,465,181**	**77%**
	Makusanyo	266,000,000	280,086,322	105%
	Jumla Kuu	**783,800,000**	**679,551,503**	**87%**
Afisi ya Hakimiliki	Mishahara na Stahiki	85,647,600	63,139,400	74%
	Matumizi Mengineyo	84,352,400	42,436,030	50%
	Jumla ya Ruzuku	**170,000,000**	**105,575,430**	**62%**
Afisi Kuu Pemba	Mishahara na Stahiki	157,792,000	117,212,000	74%
	Matumizi Mengineyo	91,499,000	37,130,310	41%
	Jumla	**249,291,000**	**154,342,310**	62%
Jumla ya Wizara (Mishahara, Stahiki na OC)		**10,244,164,000**	**6,589,077,001**	**61%**

Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2014/15

TAASISI/IDARA	ENEO LA BAJETI	BAJETI ILIOTENGWA	FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI-MACHI	ASILIMIA (%)
Jumla Mishahara		6,551,455,000	4,861,750,000	74%
Jumla Matumizi Mengine		3,692,709,000	1,727,327,001	47%
Jumla Maendeleo SMZ		1,100,000,000	315,000,000	29%
Jumla Washirika wa Maendeleo DPs		1,579,748,700	630,530,050	40%
Jumla ya Wizara Maendeleo		2,679,748,700	945,530,050	35%
Jumla Kuu ya Wizara		13,689,212,700	8,077,147,662	59%
Jumla Makusanyo		442,494,000	389,396,692	88%
Jumla Ruzuku		765,300,000	542,540,611	71%

Kiambatanisho 2: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2015/16

FUNGU/ IDARA	KAZI ZA KAWAIDA (000)					KAZI ZA MAENDELEO (000)			JUMLA KUU
	JUMLA	MSHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	UNGUJA	PEMBA	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	
14 – Mahkama Kuu	5,143,100	3,808,100	1,335,000	3,548,681	1,594,519	0	0	0	**5,143,100**
15 – Afisi ya M/ Mkuu	1,010,200	409,800	600,400	1,010,200	0	0	0	0	1,010,200
46 - Tume ya K/ Sheria	527,000	175,800	351,200	527,000	0	0	0	0	527,000
35 - Afisi ya M/Mashtaka	1,567,300	1,015,300	552,000	1,273,300	294,000	0	0	0	**1,567,300**
36/03 - Afisi Kuu Pemba	335,956	249,926	86,031	0	335,956	0	0	0	335,956
36/04 - Idara ya MSU	222,872	133,109	89,763	222,872	0	300,000	1,100,000	1,400,000	**1,622,872**
36/05 - Afisi ya Mufti	487,562	336,715	150,847	357,612	129,950	0	0	0	**487,562**
36/06 - Idara ya Uendeshaji na Utumishi	825,316	413,688	411,628	825,316	0	0	0	0	**825,316**
36/11Wakala wa UBM	308,152	173,614	134,538	290,594	17,547	1,000,000	0	1,000,000	**1,308,152**

Kiambatanisho 2: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2015/16

FUNGU/ IDARA	KAZI ZA KAWAIDA (000)					KAZI ZA MAENDELEO (000)			JUMLA KUU
	JUMLA	MSHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	UNGUJA	PEMBA	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	
36/901 - Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo	501,642	257,548	244,095	421,190	80,452		0	0	**501,642**
Ruzuku - DPP	59,800	0	59,800	0	0	0	0	0	**59,800**
Ruzuku KWNMA	587,800	393,063	194,737	453,957	133,843		0	0	**587,800**
Ruzuku-Afisi ya Hakimiliki	240,000	127,254	112,746	240,000	0	0	0	0	**240,000**
Jumla Ruzuku	**887,600**	**520,317**	**367,283**	**693,957**	**133,843**	**0**	**0**	**0**	**887,600**
Jumla G01	**2,681,500**	**1,564,599**	**1,116,901**	**1,117,584**	**563,916**	**1,300,000**	**1,100,000**	**2,400,000**	**5,081,500**
G02, G03, G04,&G05	**8,247,600**	**5,409,000**	**2,838,600**	**6,359,181**	**1,888,519**	**0**	**0**	**0**	**8,247,600**
JUMLA KUU	**11,816,700**	**7,493,916**	**4,322,784**	**9,170,723**	**2,586,277**	**1,300,000**	**1,100,000**	**2,400,000**	**14,216,700**

Kiambatanisho 3: Makusanyo ya Mapato na Makadirio ya 2015/2016

IDARA/TAASISI	MAKADIRIO 2014/15	MAKUSANYO HALISI 2014/15	%	MATARAJIO JUNI 2014	JUMLA HADI JUNI 2014	%	MAKADIRIO 2015/16
36/11 WAKALA WA USAJILI BISHARA NA MALI	126,494,000	107,139,150	85%	26,784,788	133,923,938	106%	128,711,000
14MAHKAMA	95,000,000	128,346,107	135%	32,086,527	160,432,634	169%	150,000,000
36/902 MRAJIS WA VIZAZI NA VIFO	221,000,000	153,911,435	70%	38,477,859	192,389,294	87%	245,000,000
JUMLA KUU	**442,494,000**	**389,396,692**	**88%**	**97,349,174**	**486,745,866**	**110%**	**523,711,000**

Kiambatanisho 4: Miradi ya Maendeleo 2015/16

Namba ya Mradi	Jina la Mradi	Mchango wa Serikali	Mchango wa Wahisani	Mhisani	Jumla Kuu
	Programu ya Mabadiliko ya Sekta ya Sheria	300,000,000	1,100,000,000	UNDP/EU	1,400,000,000
	Mradi wa Mageuzi ya mfumo wa usajili wa Biashara	1,000,000,000	0		1,000,000,000
	JUMLA KUU	**1,300,000,000**	**1,100,000,000**		**2,400,000,000**

Kiambatisho 5a:- Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2014/2015

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahkama	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Mahkama ya Rufaa Tanzania	6					3	3	3	3
M/Kuu Vuga	124	58		11		53	1	2	
M/Kuu Pemba	39	3				32	3	4	
Mahkama ya kazi	11	11							
M/Kadhi Rufaa Z'bar	27					27	4		
M/ Kadhi Rufaa P	7					7	3		
M/ Mkoa Vuga	72	15	1	56	2	1			
M/Mkoa Mfenesini	42	4	1	31	3			7	
Mkoa Mwera	26	0	0	26	3	0	0	0	0

Kiambatisho 5a:- Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2014/2015

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahkama	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Wilaya Konde	65	0	0	65	45	0	0	0	0
Watoto Vuga	10	0	0	10	1	0	0	0	0
Watoto Chake	11	0	0	11	4	0	0	0	0
Watoto Wete	7	0	0	7	2	0	0	0	0
Jumla	**2967**	**125**	**2**	**2703**	**1910**	**123**	**14**	**16**	**3**

Kiambatanisho 5b: Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Mwanzo na Kadhi 2014/15

Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Mwanzo						Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Kadhi		
Mahkama ya Mwanzo		Kesi za Madai		Kesi za Jinai		Mahkama za Kadhi Wilaya	Kesi za Madai	
	Jumla	Zilizo funguliwa	Zilizo amuliwa	Zilizo funguliwa	Zilizoamuliwa		Zilizofungul iwa	Zilizotolewa uamuzi
Manispaa	644			644	644			
M/kwerekwe	1396	81	13	1315	1281	Mjini	586	232
Mwera	31	4	0	27	7	Mwera	60	50
Mfenesini	240	4	0	236	198	Mfenesini	34	9
Mkokotoni	67	10	4	57	27	Mkokotoni	56	19
Makunduchi	77	18	7	59	44	Makunduchi	18	9
Chwaka	31	4	3	27	20	Chwaka	5	4
Mkoani	43	10	2	33	17	Mkoani	55	31
Kengeja	15	2	1	13	2	Kengeja	8	3
Chake chake	112	11	4	101	79	Chakechake	116	71
Wete	61	7	2	54	41	Wete	58	21
Konde	40	14	10	26	20	Konde	37	10
JUMLA	**2783**	**165**	**46**	**2618**	**2402**	**JUMLA**	**1033**	**459**

Kiambatanisho 6: Miswada – Afisi ya Mwanasheria Mkuu 2014/15

Nam	**Miswada ya Sheria iliyoandaliwa**
1.	Mswada wa Sheria ya Hati ya Uwakala
2.	Mswada wa Sheria ya Wasimamizi wa Amana na Wasia
3.	Mswada wa Sheria ya Tafsiri ya Sheria na Masharti ya Jumla
4.	Mswada wa Sheria ya Kusimamia Hundi

Kiambatanisho 7a: Mapato – Wakala wa Usajili Biashara na Mali 2014/15

Chanzo cha Mapato	Makusanyo Halisi 2013/14	Bajeti 2014/15	Makusanyo Halisi ya Miezi Tisa 2014/15	Bajeti 2015/16
Usajili wa Alama za Biashara	50,910,000	51,250,000	49,318,000	52,950,000
Usajili wa Makampuni na NGO'S	45,769,220	40,604,000	21,747,000	41,356,000
Usajili wa Majina ya Biashara	13,197,500	15,000,000	15,179,650	15,905,000
Usajili wa Nyaraka	19,435,350	19,640,000	16,731,500	18,500,000
Jumla	**129,312,070**	**126,494,000**	**102,976,150**	**128,711,000**

Kiambatanisho 7b: Mapato – Ofisi ya Mrajis Vizazi na Vifo 2014/15

ENEO LA MAPATO	ZILIZOIDHINISHWA	ZILIZOKUSANYWA	PUNGUFU	MAKADIRIO 2014/15
Estate Duty	2,000,000	0	2,000,000	2,000,000
Vizazi na Vifo	180,000,000	131,378,000	48,622,000	200,000,000
Ndoa na Talaka	36,000,000	21,988,000	14,012,000	40,000,000
Admin. General Fee	3,000,000	545,435	2,454,565	3,000,000
JUMLA	**221,000,000**	**153911435**	**67,088,565**	**245,000,000**

Kiambatisho 8: Vikundi vilivyosafirisha Mahujaji 2014 - KWNMA

S/N	JINA LA KIKUNDI	WANAUME	WANAWAKE	JUMLA
1	Ahlu Sunna Waljamaa	50	70	120
2	Ahludaawa Hajj&Travel Agency	88	82	170
3	Zanzibar Hajj Travel Agency	68	54	122
4	Tawheed	85	60	145
5	Al-Bushra	40	20	60
6	Istiqaama Hajj Mlandege	50	87	137
7	Zanzibar Istiqaama Hajj(Mother Care)	69	63	132
8	Jumaza Hajj Group	55	25	80
9	Alharamain Hajj	65	55	129
	JUMLA	**570**	**516**	**1086**

Kiambatisho 9: Usajili wa Kazi za Hakimiliki

S/N	AINA YA KAZI	IDADI YA KAZI
1	Taarab	7
2	Zenji Flaver	9
3	Qasida	79
4	Injili	10
5	Filamu	20
6	Vitabu	9
7	Miradi	1
8	Vipindi	1
9	Michoro	2
	JUMLA	**138**

Kiambatanisho: 10a Idadi ya Wafanyakazi wa Wizara 2014/2015

Idara/Taasisi	Jumla	Unguja		Pemba		Wafanyakazi Kielimu		
		W/me	W/ke	W/me	W/ke	Cheti au chini	Stashahada au zaidi	Stashahada au zaidi%
Mahkama	**391**	174	100	79	38	251	140	**36%**
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	**52**	31	21			24	28	**54%**
Tume ya Kurekebisha Sheria	**20**	12	8			11	9	**45%**
Mkurugenzi wa Mashtaka	**99**	51	26	17	5	28	71	**72%**
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	**16**	8	8			2	14	**88%**
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	**50**	29	21			32	18	**39%**
Afisi Kuu Pemba	**29**			17	12	21	8	28%
Idara ya Mufti wa Zanzibar	**43**	18	11	10	4	25	18	**42%**
Mrajis Vizazi na Vifo	**35**	6	21	5	3	23	12	**34%**
Wakala wa Usajili Biashara na Mali	**39**	20	13	4	2	17	22	**59%**
Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	**8**	4	3	1			8	**100%**
Kamisheni ya Wakfu	**86**	37	16	24	9	56	30	**35%**
Jumla	**873**	**391**	**252**	**157**	**73**	**490**	**378**	**43%**

Kiambatanisho 10b: Idadi ya Wafanyakazi Waliopo Mafunzoni 2014/15

IDARA	SHAHADA YA UZAMILI		STASHAHADA YA UZAMILI		SHAHADA		STASHAHADA YA JUU		STASHAHADA		CHETI		JUMLA
	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	
Mahkama	3	3			4	2			10	7	2	3	**34**
Afisi ya Mwanasheria Mkuu		1			1				2				**4**
Afisi ya M/ Mashtaka	1	9			3	3			3	1		1	**21**
Tume ya Kurekebisha Sheria		1			1				3				**5**
Idara ya Mipango na Sera	2					1							**3**
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1					1							**2**
Afisi Kuu Pemba		1				2					2		**5**
Afisi ya Mufti wa Zanzibar					2				3				**5**
Wakala wa Usajili Biashara na Mali		1				1			1				**3**
Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo													
Afisi ya Msajili wa Hakimiliki													
Kamisheni ya Wakfu na MA					2	1			1	2	1	3	**10**
JUMLA	**7**	**7**			**10**	**8**			**20**	**9**	**5**	**6**	**72**